JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## UCHUNGUZI WA MIPAKA NA KUGAWA MAJIMBO KWA AJILI YA UCHAGUZI MKUU WA 2015

Kwa mujibu wa Ibara ya 74(6) (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ina mamlaka ya kuchunguza mipaka na kuwagawa maeneo kwa ajili ya Uchaguzi wa Wabunge. Aidha, Ibara ya 75 (4) inaipa Tume uwezo wa kugawa majimbo mara kwa mara na angalau kila baada ya miaka kumi.

Hivyo, Tume inakusudia kuanza mchakato wa kuchunguza mipaka na kugawa majimbo kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Vigezo vitakavyotumika katika kuchunguza mipaka na kugawa majimbo ni hivi vifuatavyo:-

(i) **Mgawanyo wa Wastani wa Idadi ya Watu (Population quota)**

Hii ni idadi ya watu katika Jimbo inayopatikana kwa kuchukua idadi ya watu wote nchi nzima na kugawanywa kwa idadi ya Majimbo yaliyopo. "Population quota" itazingatia hali halisi ya idadi ya watu Mijini na Vijijini. Kigezo cha "Population quota"

ndicho kigezo kikuu cha kwanza kitakachotumika katika kuamua majimbo gani yatagawanywa. Majimbo yatakayokidhi kigezo hiki ndiyo pekee yatakayoendelea kufikiriwa kwa kuwekewa vigezo vingine. Takwimu za Idadi ya watu zitakazotumika ni za makisio mpaka mwaka 2015 na zitapatikana Ofisi ya Takwimu ya Taifa. Kwa mujibu wa takwimu "Population quota" kwa upande wa majimbo ya Mijini itakuwa 325,000 na kwa majimbo ya Vijijini ni 235,000 Tume inapenda kueleza kwamba majimbo ambayo hayajatimiza idadi hiyo ya watu wasilete maombi isipokuwa tu kama ni Halmashauri mpya.

(ii) **Idadi ya Watu**

Idadi ya watu itakayotumika ni ile iliyotokana na makisio ya ongezeko la watu hadi Julai, 2015. Majimbo yenye watu wengi yatafikiriwa zaidi. Takwimu zitapatikana kutoka ofisi ya Takwimu ya Taifa.

(iii) **Upatikanaji wa Mawasiliano**

Hapa itaangaliwa urahisi wa mwakilishi kuwafikia/kuwasiliana na anaowawakilisha katika maana ya barabara, simu, vyombo vya habari (Redio na Magazeti) Majimbo yenye mawasiliano duni yatafikiriwa kwanza.

(iv) **Hali ya Kijiografia**

Hapa itaangaliwa Jimbo liko sehemu gani; kwa mfano, maeneo ya milimani, visiwani au mabondeni. kwa lengo la kuona ni kwa jinsi gani litawakilishwa kwa ufanisi zaidi.

(v) **Hali ya Kiuchumi**

Hapa uangalifu ni kuangalia maeneo ambayo yako juu sana kiuchumi yasimeze kiuwakilishi maeneo yaliyo chini kiuchumi. Maeneo yaliyo chini kiuchumi yatafikiriwa kwanza. Takwimu zitakazotumika katika kigezo hiki za ukusanyaji wa mapato zitapatikana TAMISEMI.

(vi) **Ukubwa wa Eneo la Jimbo husika**

Ukubwa wa eneo la Jimbo utaangaliwa na majimbo yenye maeneo makubwa yatafikiriwa. Taarifa za ukubwa wa maeneo ya majimbo zitapatikana Tume ya Taifa ya Uchaguzi na OWM - TAMISEMI.

(vii) **Mipaka ya kiutawala**

Katika kugawa Majimbo Tume itazingatia mipaka ya kiutawala. Pale ambapo mipaka ya kiutawala itabadilika kabla ya Tume kufanya Ugawaji wa Majimbo, Tume itazingatia mabadiliko hayo.

(viii) **Jimbo moja lisiwe ndani ya Wilaya/Halmashauri mbili**

Kigezo hiki kitazingatiwa ili kuepusha Mwakilishi kutumikia Wilaya/Halmashauri mbili tofauti kwa wakati mmoja.

(ix) **Kata moja isiwe ndani ya Majimbo mawili**

Kigezo hiki kitazingatiwa kuepusha Diwani wa kata iliyogawanywa kutumikia Halmashauri/Wilaya mbili tofauti.

(x) **Mpangilio wa Maeneo ya Makazi ya watu yaliyopo (Existing pattern of human settlement)**

Kigezo hiki kitatiliwa maanani zaidi mpangilio wa makazi ya watu katika jimbo husika.

(xi) **Mazingira ya Muungano**

Tanzania ni nchi inayounganisha sehemu mbili, kwa hivyo ugawaji wa Majimbo utazingatia upekee wa mazingira ya Muungano.

(xii) **Uwezo wa Ukumbi wa Bunge**

Katika kugawa Majimbo Tume itazingatia pia uwezo wa ukumbi wa Bunge ili kuepuka kuzidisha idadi ya Wabunge kupita nafasi iliyoko katika ukumbi wa Bunge.

(xiii) **Viti Maalum vya Wanawake**

Katiba ya Nchi imetenga kiasi cha zaidi ya asilimia 30 kwa ajili ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum. Mwaka 2005 idadi ya viti maalum ilikuwa 30% mwaka 2010 ilikuwa 40% Hivyo katika kugawa na kuongeza Majimbo, Tume itazingatia idadi ya Wabunge wa Viti Maalum, iwapo itaendelea kuongezeka.

**Utaratibu utakaofuatwa kuwasilisha maombi ni:**

i. Maombi/mapendekezo ya kugawa majimbo au kurekebisha mipaka yatapaswa kuwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri husika ambapo yatajadiliwa katika vikao rasmi. Inashauriwa vikao hivyo vishirikishe wadau mbalimbali.

ii. Mkurugenzi wa Halmashauri atawasilisha maombi/mapendekezo kwa Katibu Tawala wa Mkoa (RAS).
iii. Katibu Tawala wa Mkoa atawasilisha maombi/mapendekezo katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa(RCC) ili kupata maoni, zaidi.
iv. Katibu Tawala wa Mkoa atawasilisha mapendekezo Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Tume inawaalika/kuwaarifu Wadau wote wenye nia ya kugawa jimbo/Majimbo yanayokidhi vigezo vilivyotajwa kuwasilisha maombi yao Tume kwa kufuata utaratibu ulioainishwa hapo juu. Maombi yote yaliyo chini ya "population quota" iliyotajwa hayatafanyiwa kazi.

**Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 31 Mei, 2015.**

Imetolewa na



**Kailima R. K**

**Kny: MKURUGENZI WA UCHAGUZI**